

Mwongozo wa Kiswahili Karatasi ya 2
Taratibu za kufundishia.

1. (i) Kuchagua shairi la kiwango cha wanafunzi wa darasa la saba.
- (ii) Kusoma shairi na wanafunzi.
- (iii) Kueleza maana ya msamiati katika shairi.
- (iv) Kutunga sentensi mkitumia msamiati huo.
- (v) Kuliimba shairi.
- (vi) Kulikariri shairi.
- (vii) Kuliigiza shairi.
- (viii) Kutumia nyenzo.
- (ix) Kuchambua shairi
- (x) Kueleza uhuru wa shairi
- (xi) Kueleza matumizi ya tamathali za usemi katika shairi.

(zozote 9×2 = alama 18)

2. (a) Ufaafu wa mjadala.

- (i) Mwanafunzi hupata ujasiri wa kuzungumza mbele ya hadhira.
- (ii) Hukuza stadi ya kusikiliza na kuongea.
- (iii) Husaidia kurekebisha matamshi ya wanafunzi.
- (iv) Hukuza uwezo wa kufikiria kwa kina.
- (v) Humwezesha mwanafunzi kupanga hoja na kuziwakilisha kimantiki.
- (vi) Hukuza uwezo wa kutumia lugha ya kushawishi.
- (vii) Hutoa changamoto kwa wanafunzi kuheshimu maoni yaliyotofauti na yao.
- (viii) Hukuza ushirikiano kati ya wanafunzi.
- (ix) Hukuza utangamano miongoni mwa wanafunzi.
- (x) Huwasisimua wanafunzi darasani.
- (xi) Huwasaidia wanafunzi kurekebisha makosa yao wakati wa mazungumzo.

(zozote 9×1 = alama 9)

(b) Udhaifu wa mhadhara

- (i) Humnyima mwanafunzi fursa ya kushiriki katika mada.
- (ii) Humnyima mwanafunzi kukuza vipawa vyao.
- (iii) Mwalimu hawezi kutathmini wanafunzi wakati wa kipindi.
- (iv) Hufaidi wanafunzi werevu pekee.
- (v) Humnyima mwanafunzi nafasi ya kukuza kipawa cha kuzungumza.
- (vi) Hufanya mada kuwa finyu kwa sababu wanafunzi hawachangii.
- (vii) Hufaidi wanafunzi wa madarasa ya juu pekee.
- (viii) Mwalimu hawezi kubaini matatizo ya wanafunzi.
- (ix) Hufanya funzo likose uchangamfu.
- (x) Mwalimu hatumii nyenzo wakati wa funzo.
- (xi) Mwanafunzi hunyimwa nafasi ya kuuliza na kujibu maswali.

(zozote 8×1 = alama 8)

3. Andalio la somo (alama 1)

SHULE	GREDI	SOMO	TAREHE	WAKATI	IDADI
$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$	$\frac{1}{2}$

Mada	(alama 1)
Mada ndogo	(alama 1)
Matokeo maalum yanayotarajiwa	(alama 2)
Maswali dadisi	(alama 1)
Umilisi wa kimsingi unaokuzwa	(alama 1)
Maadili	(alama 1)
Nyenzo	(alama 2)
Mpangilio wa somo	(alama 1)
Utangulizi	(alama 1)
Utaratibu wa somo.	(alama 2)
Hitimisho	(alama 1)
Muhtasari	(alama 1)
Maoni/akisi	(alama 1)